**BENKI KUU YA TANZANIA**
16 Barabara ya Jakaya Kikwete
S. L. P. 2303
40184 DODOMA
**TANZANIA**
Simu: +255 22 223 3167
Barua Pepe: botcommunications@bot.go.tz

**BANK OF TANZANIA**
16 Jakaya Kikwete Road
P.O. Box 2303
40184 DODOMA
**TANZANIA**
Phone: +255 22 223 3167
Email: botcommunications@bot.go.tz

**19 Januari 2024**

# Tamko la Kamati ya Sera ya Fedha

Kamati ya Sera ya Fedha (*MPC*) ilikutana tarehe 18 Januari 2024. Mkutano huo ni wa kwanza kwa Kamati hiyo kwa kipindi ambacho Benki Kuu imeanza kutekeleza Sera ya Fedha kwa kutumia Mfumo wa Riba. Katika mkutano huo, Kamati ilibainisha kuwa mabadiliko ya utekelezaji wa Sera ya Fedha kwa kutumia mfumo wa riba badala ya ujazi wa fedha ni hatua muhimu katika maboresho ya sekta ya fedha na uchumi kwa ujumla. Mfumo huu wa kutumia riba unatarajiwa kuongeza ufanisi katika utekelezaji wa Sera ya Fedha. Aidha, mabadiliko haya yanaendana na makubaliano ya Itifaki ya Kuanzisha Umoja wa Fedha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki, ikiwa ni mojawapo ya hatua kuelekea kuwa na Sarafu Moja na Benki Kuu Moja ya Afrika Mashariki.

Kufuatia kuanza utekelezaji wa mfumo huu mpya, Kamati imefanya tathmini ya mwenendo wa uchumi na mwelekeo wake, na kuamua **Riba ya Benki Kuu, ambayo pia itajulikana kama "*Central Bank Rate*" kuwa asilimia 5.5 kwa robo ya kwanza ya mwaka 2024.** Kiwango hiki cha Riba ya Benki Kuu kinaendana na malengo ya kuhakikisha kuwa mfumuko wa bei unabakia ndani ya lengo la asilimia 5 na kuongeza kasi ya ukuaji wa uchumi kufikia lengo la asilimia 5.5 au zaidi kwa mwaka 2024. Aidha, riba hiyo imezingatia lengo la kuhakikisha thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni inaendelea kuwa imara. Ili kuwezesha kufikiwa kwa malengo haya, Benki Kuu itatumia nyenzo mbalimbali za sera za fedha kuhakikisha riba katika soko la fedha baina ya benki hapa nchini (interbank market) inakuwa tulivu. Hivyo, Benki Kuu itakuwa inafuatilia mwenendo wa riba ya mikopo ya siku 7 katika soko hilo na kuchukua hatua kuhakikisha mabadiliko ya riba hiyo yanakuwa ndani ya wigo usiozidi asilimia 2 chini au juu (+/-2) ya Riba ya Benki Kuu.

## Mwenendo wa Uchumi na Mwelekeo wake

Kamati imetathmini mwenendo wa uchumi wa dunia na hapa nchini, pamoja na mwelekeo wake, kama ifuatavyo:

**Uchumi wa Dunia**

i. Ukuaji wa uchumi wa dunia haukuwa wa kuridhisha katika robo ya mwisho ya mwaka 2023. Hali hii inatarajiwa kuendelea katika robo ya kwanza ya mwaka 2024 kutokana na migogoro ya kisiasa inayoendelea Mashariki ya Kati na vita kati ya Urusi na Ukraine. Aidha, utekelezaji wa sera ya fedha unaolenga kupunguza ukwasi, hususan katika nchi zilizoendelea, na kutotabirika kwa mazingira ya kiuchumi duniani kunatarajia kupunguza kasi ya ukuaji wa uchumi wa dunia.

ii. Mfumuko wa bei uliendelea kupungua katika nchi nyingi, kutokana na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi katika nchi mbalimbali. Katika nchi zilizoendelea, mfumuko wa bei umebaki kuwa juu ya lengo la asilimia 2, licha ya kupungua. Hali hii inatarajiwa kuendelea katika robo ya kwanza ya mwaka 2024. Hivyo, benki kuu zinatarajiwa kuendelea na utekelezaji wa sera ya fedha ya kupunguza ukwasi, japo kwa kasi ndogo tofauti na hapo awali. Katika nchi nyingi za EAC na SADC, mfumuko wa bei ulikuwa ndani ya malengo.

iii. Bei za bidhaa katika soko la dunia zilipungua katika robo ya mwisho ya mwaka 2023 ukilinganisha na kipindi kama hicho mwaka jana. Hali hii ilitokana na ongezeko la upatikanaji wa bidhaa. Bei ya mafuta ya nishati ilipungua kutokana na kupungua kwa mahitaji katika baadhi ya nchi. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2024, bei ya mafuta ya nishati inatarajiwa kuendelea kupungua. Hata hivyo, hali hii inaweza kubadilika endapo nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi (OPEC+) zitatekeleza uamuzi wao wa kupunguza uzalishaji. Aidha migogoro ya kisiasa inayoendelea Mashariki ya Kati na vita kati ya Urusi na Ukraine inaweza kuchangia hali hiyo.

**Mwenendo wa Uchumi wa Tanzania**

iv. Ukuaji wa uchumi uliimarika katika mwaka 2023. Katika robo ya tatu, uchumi ulikua kwa asilimia 5.3, na unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.4 katika robo ya nne. Kutokana na hali hii, makadirio ya ukuaji wa asilimia 5 kwa mwaka 2023 yatafikiwa. Uchumi wa Zanzibar ulikua kwa asilimia 7, na matarajio ya ukuaji wa asilimia 7.1 kwa mwaka 2023 yanaweza kufikiwa. Mwenendo huu unatokana na ongezeko la uzalishaji katika sekta mbalimbali kutokana na uboreshaji wa mazingira ya biashara na uwekezaji wa serikali hususan katika miundombinu. Katika robo ya kwanza ya mwaka 2024, uchumi wa Tanzania Bara unatarajiwa kukua kwa asilimia 5.2.

v. Mfumuko wa bei umeendelea kupungua kufikia asilimia 3 mwezi Desemba 2023 kutoka asilimia 3.2 mwaka uliopita. Kwa upande wa Zanzibar, mfumuko wa bei umepungua hadi asilimia 5.5 kutoka asilimia 8.1. Hali hii ilitokana na utekelezaji wa sera ya fedha na ya kibajeti na uwepo wa chakula cha kutosha nchini. Mfumuko wa bei unatarajiwa kuendelea kuwa tulivu kufikia takribani asilimia 3.2 katika robo ya kwanza ya 2024. Hata hivyo, hali hii inaweza kubadilika endapo nchi zinazozalisha mafuta kwa wingi (OPEC+) zitatekeleza uamuzi wao wa kupunguza uzalishaji. Aidha migogoro ya kisiasa inayoendelea Mashariki ya Kati na vita kati ya Urusi na Ukraine inaweza kuchangia hali hiyo.

vi. Ukuaji wa ujazi wa fedha ulipungua katika robo ya mwisho ya mwaka 2023. Ukuaji wa ujazi wa fedha (M3) ulipungua hadi asilimia 14.1, lakini ulibaki juu ya lengo la mwaka la asilimia 10.1. Ukuaji wa mikopo ya sekta binafsi uliendelea kuwa imara, kufikia asilimia 17.1 ukilinganisha na makadirio ya asilimia 16.4 kwa mwaka. Hali hii ilitokana na utekelezaji wa sera ya fedha iliyolenga kudhibiti viashiria vya mfumuko wa bei na kuchangia kuimarisha thamani ya Shillingi dhidi ya fedha za kigeni.

vii. Sekta ya fedha imeendelea kuwa imara. Sekta ya kibenki ilikuwa na ukwasi, na mtaji wa kutosha. Amana na mikopo imeendelea kuongezeka. Mikopo chechefu iliendelea kupungua kufikia asilimia 4.3 mwezi Desemba 2023 kutoka asilimia 5.8 mwaka 2022. Kiwango hiki kilikuwa chini ya lengo la asimilia 5. Hali hii inaashiria kupungua kwa vihatarishi vya mikopo kutokana na kuimarika kwa mazingira ya kiuchumi na jitihada zinazofanyika katika kukabiliana na vihatarishi hivi.

viii. Utekelezaji wa bajeti ulikuwa wa kuridhisha. Katika nusu ya kwanza ya mwaka 2023/24, mapato ya Serikali yalifikia takribani asilimia 96 ya lengo kwa upande wa Tanzania Bara. Kwa upande wa Zanzibar, mapato yalifikia asilimia 99.1 ya lengo. Mafanikio haya yalitokana na maboresho katika usimamizi wa mapato na utekelezaji wa mikakati ya ulipaji kodi kwa hiari. Mapato yanatarajiwa kuendelea kuongezeka kutokana na hatua zinazochukuliwa kuongeza wigo na usimamizi wa kodi. Serikali itaendelea na utaratibu wa kufanya matumizi kulingana na mapato.

ix. Sekta ya nje iliendelea kuimarika, licha ya kukabiliwa na changamoto zilizotokana na mwenendo wa uchumi wa dunia. Nakisi ya urari wa biashara nje ya nchi ilipungua kutokana na kuongezeka kwa shughuli za utalii na mauzo ya bidhaa nje ya nchi. Akiba ya fedha za kigeni imeendelea kuwa ya kutosha, ambapo ilifikia dola za Marekani bilioni 5.5 mwishoni mwa Desemba 2023. Kiwango hiki kilitosheleza kuagiza bidhaa na huduma nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi minne na nusu. Thamani ya

Shilingi dhidi ya dola ya Marekani iliendelea kuwa imara, ikipungua kwa asilimia 7.8 kwa mwaka. Sekta ya nje inatarajiwa kuendelea kuimarika katika robo ya kwanza ya 2024.

Kamati ya Sera ya Fedha imeridhishwa na mwenendo wa thamani ya shilingi dhidi ya fedha za kigeni katika siku za hivi karibuni, licha ya kuwepo kwa changamoto katika uchumi wa dunia. Kamati imesisitiza umuhimu wa kuendelea kufanya jitihada katika kuboresha soko la jumla la fedha za kigeni nchini na kuhakikisha thamani ya Shilingi inaendelea kuwa imara.

***Riba ya Benki Kuu kwa robo ya pili ya mwaka 2024 itatangazwa mwezi Aprili mwaka huu, kulingana na kalenda ya mikutano ya Kamati ya Sera ya Fedha itakayotolewa hivi karibuni*.**

**EMMANUEL M. TUTUBA**
**GAVANA**
**BENKI KUU YA TANZANIA**